***Maombi ya Cheti cha Kuzaliwa***

Usajili wa kuzaliwa unaweza kufanywa katika:

i. Katika kituo cha tiba au ngazi ya kitongoji kwa watoto wachanga (ndani ya siku 90)
ii. Katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya (usajili wa kuchelewa)
iii. Kwa mtandao (usajili wa kuchelewa, kubadilisha cheti cha zamani kuwa kipya)

Mtoto anasajiliwa mara tu baada ya kuzaliwa katika kituo cha tiba ambapo tukio la kizazi limetokea au katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata kwa vizazi vya nyumbani. Ikiwa kwa sababu fulani mtu anakosa kusajili mahali hapo, mtoto anaweza kusajiliwa wakati wa chanjo ndani ya siku 90. Aidha, tukio la kuzaliwa linaweza kusajiliwa kama usajili wa kuchelewa katika Ofisi ya Katibu wa Wilaya kwa kupitia mtandao.

***Mahitaji ya jumla kwa maombi ya cheti cha kuzaliwa:***

Mwombaji lazima aambatishe baadhi ya hati mbili kati ya zifuatazo:

• Kadi ya Kliniki ya Mama

• Kadi ya Kliniki ya Mtoto

• Tangazo la kuzaliwa

• Cheti cha Ubatizo cha Mtoto (kwa wale walio batizwa wakiwa na umri mdogo)

• Cheti cha Kumaliza elimu (Shule za Msingi au Sekondari - O Level)

• Pasi ya kusafiria

• Kadi ya mpiga kura

• Cheti cha ubatizo

**Pamoja na mojawapo ya haya:**

• Kitambulisho cha Kitaifa cha mzazi/mlezi

• Hati ya kusafiria ya mzazi

• Utambulisho kutoka Mtendaji wa Kata

N.B: Uhitaji wa kuweka vitambulisho vya wazazi vitatumika ikiwa wazazi wapo hai.

**USAJILI UNAVYOFANYIKA KWA WATOTO WACHANGA**

Mwombaji (Mzazi/mlezi) atasajili tukio hili kwenye dawati la Usajili katika Kituo cha tiba kizazi kilipotokea wakati mtoto anapozaliwa au wakati wa kupata chanjo. Pia Usajili unaweza kufanyika katika ofisi ya kata kwa vizazi vya nyumbani.

***Mwombaji atatakiwa kuwa na nakala laini (soft copies) za viambatanisho vinavyotakiwa kuwa katika mfumo wa pdf kwa ajili ya kuviambatanisha pamoja na maombi yake katika mfumo nyaraka hizo ni kama zifuatavyo;***

• Kadi ya Kliniki ya Mama

• Kadi ya Kliniki ya Mtoto

• Tangazo la kuzaliwa

- Cheti cha Ubatizo cha Mtoto (kwa wale walio batizwa wakiwa na umri mdogo)
- Cheti cha Kumaliza elimu (Shule za Msingi au Sekondari - O Level)
- Pasi ya kusafiria
- Kadi ya mpiga kura
- Cheti cha ubatizo

**Pamoja na mojawapo ya haya:**

- Kitambulisho cha Kitaifa cha mzazi/mlezi
- Hati ya kusafiria ya mzazi
- Utambulisho kutoka Mtendaji wa Kata

N.B: Uhitaji wa kuweka vitambulisho vya wazazi vitatumika ikiwa wazazi wapo hai

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

(i) Ada ya utoaji wa cheti kupitia mfumo kwa matukio ya vizazi yaliyosajiliwa ndani ya muda Tshs 7000

(ii) Ada ya usajili wa kizazi kilichochelewa kuandikishwa ni Tsh 8,000 kwa tukio lililo chini ya miaka 10 na Tsh 20,000 kwa tukio zaidi ya miaka 10.

***Mwombaji atatakiwa kuwa na nakala laini (soft copies) ya cheti chake cha kuzaliwa kinachotakiwa kuwa katika mfumo wa pdf kwa ajili ya kuambatanisha pamoja na viambata viwili kati ya vifuatavyo:***

� Kadi ya Kliniki ya Mama

� Kadi ya Kliniki ya Mtoto

� Tangazo la kuzaliwa

� Cheti cha Ubatizo cha Mtoto (kwa wale walio batizwa wakiwa na umri mdogo)

� Cheti cha Kumaliza elimu (Shule za Msingi au Sekondari - O Level)

� Pasi ya kusafiria

� Kitambulisho cha NIDA

� Kitambulisho cha Mpiga kura

**Pamoja na mojawapo ya haya:**

� Kitambulisho cha Kitaifa cha mzazi/mlezi

� Hati ya kusafiria ya mzazi

N.B: Hii itatumika ikiwa wazazi wapo hai

***MAOMBI YA KUFANYA MAREKEBISHO KATIKA VYETI VYA KUZALIWA***

Huduma hii kwa sasa haipo kieletroniki na hivyo kuhitaji mwombaji kufika katika Ofisi zetu za Makao Makuu au Wilaya.

Marekekbisho ya Jina la Mtoto

Marekebisho katika ya Sheria Usajili wa Vizazi na Vifo Sura ya 108 yaliyofanyika mwaka 2019, na kuruhusu marekebisho ya majina ya mtoto pale ambapo kizazi kilisajiliwa kabla ya kupewa jina au kizazi kilisajiliwa na kupewa jina lakini jina hilo limebadilishwa, mzazi au mlezi anaweza, muda wowote kabla mtoto hajafikisha miaka 18 kupeleka maombi kwa Msajili ya kutaka jina libadilishwe.

Maombi hayo yatawasilishwa kwa barua kwa Msajili Mkuu na kuambatisha nyaraka za uthibitisho pamoja na kulipia ada iliyowekwa, na endapo maombi yatakidhi vigezo marekebisho hayo yatafanyika katika daftrari la usajili.

Angalizo; Jina linalobadilika ni la mtoto na sio majina ya wazazi.

Marekebisho ya herufi kwenye cheti cha kuzaliwa

Marekebisho ya herufi zilizokosewa kwenye cheti yanawezekana kufanyika kwa mwombaji kuwasilisha barua na viambatisho vinavyoonesha usahihi wa taarifa zake ili aweze kufanyiwa marekebisho kama yatakidhi vigezo. Endapo jina lililokosewa ni la mzazi mwombaji awasilishe kitambulisho cha mzazi husika, kama taarifa ni za mwombaji mwenyewe atawasilisha vitambuliisho vyake mfano cheti cha ubatizo, kadi la Klinik, vyeti vya shule N.K.

**MAHITAJI YA JUMLA**

- Barua ya kuomba marekebisho
- Cheti halisi kinachotakiwa kurekebishwa
- Viambata vinavyothibitisha marekebisho yanayohitajika kama jina lililokosewa ni la mzazi utakuja na kitambulisho cha mzazi husika kama taarifa ni zako utakuja na vitambuliisho vyako mfano cheti cha ubatizo, kadi la clinic, vyeti vya shule.
- Affidavit inaweza kuhitajika
- Ada ya malipo ya shilingi 13,000/=

**UTAMBUZI WA CHETI CHA KUZALIWA KILICHOTOKEA NJE YA NCHI**

Usajili wa Kizazi hufanyika katika nchi ambayo kizazi hicho kimetokea bila kujali asili ya mtoto. Nchi husika ambapo tukio la kizazi limetokea inawajibika na kulazimika kimataifa kutoa nyaraka ya kutambua tukio hilo. Ili ombi lako liweze kufanyiwa kazi inabidi uambatanishe viambatisho vifuatavyo;

1) Cheti cha kuzaliwa kilichotolewa na mamlaka za usajili mahali ambapo mtoto amezaliwa au kadi la kliniki au taarifa za kitabibu kutoka hospitali aliyozaliwa mtoto

2) Pasi ya kusafiria ya mtoto pamoja na vitambulisho vya wazazi.

3) Cheti kilichoandikwa kwa lugha ngeni kitafsiriwe kwenda Kiswahili na Baraza la Kiswahili Tanzania.

4) Ada ya shilingi 6,000/=

N: B Barua ya utambuzi itatolewa baada ya siku 3-5 za kazi.